# MAISHA YA WATAKATIFU MAKARI



## Jinsi yalivyoandika wa Rufinus na Palladius na wengine

**Tafsiri ya Padri Etienne Sion, M.afr.**

**Kipigo cha chapa Mtandao**
**2020**

**Agape Publications**
**P.O.Box 76021 Dar-es-Salaam**

**Simu : + 255 767 342068**
e-mail : kungwecentre@gmail.com
kungwecentre@outlook.com

# Utangulizi

Jina la Makari ni jina maarufu katika historia ya watawa walioishi jangwani mwa Misri. Tunamkuta mmoja aliyekuwa mfuasi wa Mt. Antoni na aliyemhudumia miaka kumi na mitano katika uzee wake. Huyu alikuwa mmojawapo aliyemzika Mt. Antoni. Mwingine alikuwa Mt. Isaka wa Fayoun aliyeambiwa na Bikira Maria kwenda kumwona Baba Antoni kupata baraka zake kabla hajaenda kwa njia ya mababa. Baada ya Mt. Antoni kufariki Makari huyu alishika nafasi yake ya kuwaongoza watawa.
Lakini miongoni mwa wakaa pweke katika nchi ya Misri wawili wamesifiwa sana kuliko wenzao walioitwa kwa jina hilo. Wote wawili walikuwa mashujaa wa Yesu Kristo wasioshindwa. Wote wawili walipadirishwa. Na wote wawili waliishi wakati wa Mt. Antoni, pengine walikuwa wafuasi wake. Hapa hatuna uhakika wa kutosha.
Mmoja wao, aliyetangulia kuzaliwa, alikaa karibu ya mji wa Theba, upande wa Kusini ya Misri. Alikuwa na fadhila bora na mwenendo wake ulikuwa wa ajabu kweli. Makari huyu huitwa mara nyingine Makari mkubwa kwa sababu alimtangulia mwenzake kuzaliwa au huitwa Makari Mmisri.
Makari mwingine anaitwa Makari Mdogo kwa sababu amezaliwa nyuma ya mwenzake. Makari Mdogo huyu alizaliwa katika mji wa Aleksandria, mnamo mwaka kama 310 B.K., yaani, baada ya kuzaliwa kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Kwa hivi watu wengine walimwita jina lake Makari Mdogo au Makari wa Aleksandria au Makari mkaa mjini.

Habari zao zinapatikana katika maandishi ya Rufinus, Askofu Palladius na Mt. Hieronimo.[1] Sehemu sehemu nimetumia tafsiri ya Pd. Heribert Meyer kuhusu maisha ya Makari mdogo, lakini ilinibidii kubadilisha mpango wake, kwa sababu mara nyingi aliyoyasimulia kwa Makari mdogo, yanasimuliwa pia kwa Makari mkubwa na mmoja wa Waandishi waliotajwa hapo juu.

[1] Palladius, alikuwa askofu wa Helenopolis. Aliandika : *The Laudiac History*, na Rufinus, *Sayings of the Desert Fathers*. Palladius alikuwa mfuasi wa Makari wa Aleksandria kwa miaka tisa kabla ya kuwa Askofu.

Fr. Etienne Sion, M.afr.

# Sura ya 1
# Maisha ya Makari mkubwa

Makari mkubwa alizaliwa Misri, mnamo mwaka 300 B.K. Alipokuwa bado kijana akaenda kuishi katika kijumba, karibu na kijiji chake. Akaanza kumtumikia Mungu kwa ukamilifu sana, hadi kusifiwa na wote walioishi karibu naye, hata Askofu alitazamia kumpatia daraja ndogo. Kwa unyenyekevu, akikataa kazi hiyo, akakimbia mahali pengine, karibu na mji fulani, na huko akaitikia mwito wake kuishi kama mkaa pweke. Daima kwa mikono alifanya kazi, lakini kwa moyo aliongea na Mungu. Ikatokea kwamba mtu mmoja wa mjini alipoona jinsi alivyoishi alimwendea ili amsaidie kuuza vikapu vyake na kumhudumia. Akawa kama boi wake.
Wakati ule, katika mji wa jirani, Shetani alimfundisha kijana mmoja kumtongoza msichana na kutenda naye dhambi kwa siri. Msichana alipojulikana kuwa na hali nyingine aliulizwa na wazazi wake, akawajibu akasema: “Makari mkaa pweke yule aliyehamia hapa amenikosesha!“
Basi wenyeji wote wakamwendea Makari upwekeni kwake wakamghadhibikia vibaya wakapiga kelele sana njiani. Wakamkamata wakamvuta mjini wakamwaibisha sana. Walichukua vyungu vya kupikia na mitungi iliyoharibika. Wakaifunga kamba na wakamfugia Makari shingoni mwake. Wakapita naye katika njia zote za mji wao wakimpiga na kumtukana na kila wakati wakatangaza wakasema: “Mtawa huyu ameharibu msichana wetu! Mpigeni! Mpigeni!“ Siku hiyo Makari akateswa vibaya kweli.
Boi wake akamfuata Makari kwa mbali kwa kuwa hata yeye alisumbuliwa nao. Wakamwambia kwa ukali na kwa dharau wakisema: “Tazama, wewe kila mara umemsifu mkaa pweke wako huyu kwamba ni mtu mwema sana. Kumbe ni mnafiki tu na mtongozaji!“
Basi wakakutana na mkaa pweke mwingine aliyekaa karibu ya mji ule. Huyu akawaambia akasema: “Acheni kumpiga mtawa mgeni huyu!“ Baba wa msichana akasema: “Sitamwacha mtawa huyu mpaka atakapomleta mdhamini wa riziki za mtoto wetu!“. Makari akamwomba mwenyeji yule aliyekuwa boi wake awe mdhamini wake. Mtu huyu akakubali, maana amejua kuwa Makari ni mtu mwema kweli. Ndipo Makari alipoachiliwa. Akarudi kijumbani kwake akatoa mikeka na vikapu vyote akampa mdhamini wake. Huyu akaviuza akachukua fedha zile akampelekea msichana yule aliyemsingizia mkaa pweke.

Makari mwenyewe akajihimiza kufanya kazi kwa bidii sana akasema nafsini mwake: “Tazama, Makari, umepata mwanamke! Kwa hivi yakupasa kufanya kazi nyingi zaidi, ili umlishe vizuri na kumpa mavazi!“ Siku zote akafanya kazi mchana kutwa mpaka usiku. Akampelekea msichana yule fedha zote alizochuma kwa taabu zake.
Zilipotimia siku za msichana kwa kumzaa mtoto alitaabika vibaya sana. Siku kadha wa kadha alikuwa na uchungu wa kuzaa asipate mtoto. Mama yake akamwuliza sababu, naye msichana akajibu akasema: “Ninaijua mimi mwenyewe, basi!“ Lakini mama yake hakuridhika na majibu haya akamwuliza mara ya pili kwa nguvu kweli. Basi msichana akaungama akasema: “Nimemsingizia mkaa pweke yule bure na nimemshtaki kwa uongo. Mtawa huyu hakunitongoza wala hakunikosesha. Ni kijana fulani aliyenitia mimba hii!“
Habari hii ikaenea upesi mjini mle. Hata boi wa Makari akaisikia. Akafurahi sana kwa sababu sifa nzuri ya mkaa pweke imepatikana tena. Akamwendea upesi sana Makari upwekeni kwake akamwambia akasema: “Baba, msichana yule aliyekusingizia uongo ameshindwa kuzaa mpaka alipokubali kwamba amekushtaki kwa uongo na kwamba wewe hukumkosesha hata kidogo. Tazama, watu wa mji wote wako njiani kukufikia wewe. Wanataka kuomba radhi kwako kwa sababu siku ile walikuaibisha bure.“
Makari aliposikia maneno ya boi wake alisimama upesi akachukua vitu vyake vichache akakimbia akahamia jangwa la Shete, maana hakupenda kusifiwa na watu wale. Alikuwa na umri wa miaka kama thelathini. Hakuna mtu aliyeishi katika jangwa la Shete kabla ya Makari. Lilikuwa eneo kubwa la mchanga wenye moto. Maji hayakupatikana, isipokuwa katika mashimo machache, yenye harufu baya. Huko Makari akaweka misingi ya maisha ya ukamilifu, ambayo yeye mwenyewe akafika na wengi pamoja naye. Watu walianza kumfuata na kujiweka chini ya uongozi wake. Makari alipokaa miaka kumi tu katika jangwa la Shete, wanafunzi wake wakawa wengi, ikawa lazima kupata padri kuwalisha kwa Neno la Mungu na kwa Mwili na Damu ya Yesu Kristo. Makari akalazimishwa kupadirishwa na kuwatenda watawa kama padri. Alijaliwa na Mungu karama nyingi, kuwafukuza pepo wachafu, karama ya unabii, na kuyajua mambo yatakayotokea.
Palladius anatusimulia jinsi Makari alivyomwonya juu ya tamani ya mali, mfuasi wake Yohane, ambaye baadaye alipadirishwa na kushika nafasi yake. Alimwambia kwamba kama hajirekebishi mapema kushinda udhaifu wake ataadhibiwa kama Gehazi. Na ndivyo ilivyotokea miaka kumi na mitano au ishirini baada ya kifo cha Makari. Yohane alipochukua mali ya maskini kwa

ajili yake mwenyewe, akashikwa vibaya sana na ukoma, hata mwili wake wote ulikuwa vidonda vitupu, na hakupatikana mahali pa kuwekwa kidole. Palladius pia anatusimulia uwezo wake juu ya pepo wachafu. Palikuwa na Mmisri mmoja aliyempenda mke wa mtu fulani. Aliposhindwa kumtongoza akamwendea mganga asilia na kusema: “Umwongoze anipende, au kumfanya mume wake amfukuze“. Mganga alipopokea fedha nyingi akatumia ufundi wake kumbadilisha mwanamke huyu kuwa punda. Mume wake aliporudi akashangaa kuona kwamba punda amejilaza katika kitanda chake. Akalia na kulalamika. Akaongea na punda lakini hakupata jibu. Akawaita Mapadri wa kijiji kile na kuwawonyesha mke wake, lakini ilibaki fumbo kwao. Kwa muda wa siku tatu hakula majani, chakula cha punda, wala mkate, chakula cha binadamu. Mwishowe, ili Mungu atukuzwe kwa njia ya Makari, mume wake akamtia hatamu kinywani mwake, kama wanavyofanya kwa farasi, na kumwongoza jangwani mpaka kufika kwa Makari. Walipokaribia kijumba chake, watawa waliokaa na Makari, wakashindana na punda na kumwambia mwanaume: “Kwa nini unatuletea punda wako hapa?“ Akawajibu: “Ili Makari amhurumie“. Wakamwambia: “Kulikoni?“ Mume wake akawajibu: “Huyu ndiye mke wangu aliyebadilishwa kuwa punda, na leo ni siku ya tatu tangu alipoonja chakula. “Basi wakamwambia Makari aliyekuwa anasali, kwa sababu Mungu alikwisha kumfunulia habari hii na alikuwa anamwombea. Kwa hiyo Makari akawajibu watawa: “Ninyi ni punda, kwa sababu mna macho ya punda. Mwanamke huyu hakubadilishwa, isipokuwa kwa macho ya watu waliodanganywa. “Akabariki maji na kumwagia mwilini mwake. Mara akaonekana kwa wote kama mwanamke. Baada ya kumpatia chakula, mwanamke akarudi pamoja na mume wake nyumbani wakimshukuru Mungu. Makari akamwambia mwanamke: “Usiache kuhudhuria kanisani, wala kupokea komunio. Mambo hayo yote yalikupata kwa sababu hakuhudhuria kanisani wala kukomunika kwa wiki tano.“ [2]




---

[2] From Palladkius : *The Laudiac History*, Macarius of Egypt 1.

Wakati wengine Makari aliletewa na wazazi wake msichana mdogo ambaye sehemu zake za siri ziliharibika kabisa. Nyama ililiwa kwa kiasi kwamba undani ya mwili wake ulionekana wazi, na funza nyingi zilikuwa zinatoka kwa njia ile. Watu hawakuweza kuvumulia kukaa karibu naye kwa sababu ya harufu mbaya kutoka kwa mwili wake. Makari alimhurumia bikira huyu mwenye mateso makali. “Jipe moyo, mwanangu“ alimwambia, “Bwana anataka uvumilie jambo hilo kwa ajili ya wokovu wako na siyo kwa ajili ya hukumu yako.  Naona kwamba kupona kwako kutakuokoa na hatari.“
Akaanza kumwombea kwa siku saba mfululizo. Baadaye akayabariki mafuta na kumpaka viungo vyake na kumrudisha afya yake. Hakuonekana kuwa tena msichana bali kuwa mvulana na akashika nafasi yake kati ya wanaume.
Pia inasemekana kwamba Mmisri mmoja alikuwa na mwana aliyepooza. Akampeleka kwa kijumba cha Makari, na kumwacha mlangoni pake, akilia sana. Yeye akakaa mbali. Mzee Makari alipotoka alimwona kijana na akamwuliza: “Nani amekuleta hapa?“ Kijana akamjibu: “Baba yangu amenileta hapa na akaondoka“. Mzee akamwambia: “Simama na nenda kukaa naye“. Kijana mara akasimama na akaenda kwa baba yake.
Siku nyingine kijana aliyepagawa na pepo akaletwa kwa Makari na mama yake, akifungwa na wanaume wawili. Shetani alikuwa na mbinu zake kufanya kazi. Baada ya kula vipande vitatu vya mkate na kunywa bilauri moja ya maji, kijana alikuwa anatema chakula na kukiyeyusha kiwe mvuke. Kwa njia hiyo yote aliyokula na kunywa yaliyeyushwa kama kwa moto. Kuna aina ya pepo ambao wanaitwa pepomoto, kwa sababu kuna tofauti kati ya pepo, kama kuna tofauti kati ya wanadamu, siyo ki-hali bali ki-tabia. Kwa hiyo mama yake alikuwa analia na kumsihi Makari kumwombea. Makari akamchukua kijana na kumwombea kwa Mungu. Baada ya siku mbili tatu, ugonjwa ulipotulia kidogo, Makari akamwambia mama yake: “Kiasi gani cha chakula unataka ale?” Akamjibu: “Mikate mitatu”. Baada ya kumkemea kwa sababu kiasi hiki kilikuwa mno, na kumwombea tena, akiwa amefunga siku saba, alimpatia utaratibu wa kula mkate mmoja, na lazima kufanya kazi. Alipoponywa akamrudisha kwa mama yake.
Ajabu nyingi zikafanyika kwa mikono ya Makari. Siku moja ilitukia kuwa mwenyeji wa ujirani wa Makari aliuawa. Marehemu alipokwisha zikwa mtu wa bure alisingiziwa kuwa mwuaji. Huyo akakimbia pangoni kwa Makari. Washindani wake wakamfuata mle mle wakamfunga kamba wakataka kumpeleka barazani apate adhabu yake. Mfungwa akaapa viapo kwamba hakumwua mwenzake. Wakazozana kwa makelele pale pangoni kwa Makari muda mrefu. Basi Makari aliyesikia yote akasimama akawauliza: “Wapi mmemzika mareheumu huyu aliyeuawa?“ Wakamwambia mahali alipozika.

Basi Makari akafuatana nao mpaka kwenye kaburi. Pale akapiga magoti akasali. Halafu aliwaambia watu wale akasema: “Sasa hivi Bwana mwenyewe ataonyesha kama mfungwa wenu amemwua marehemu wenu!“ Akapaza sauti akamwita marehemu kwa jina lake. Watu wote waliokusanyika pale wakasikia kuwa marehemu ameitika jina lake mle mle kaburini. Makari akamwambia akasema kwa sauti kubwa: “Ninakutaja kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo: utuambie kama umeuawa na mtu huyu aliyefungwa na anayetiwa hatiani!“ Watu wote wakasikia tena maneno aliyosema marehemu kaburini: “La, mtu huyu hakuniua!“

Basi wote wakastaajabu. Wakamwomba Makari amwulize marehemu jina la mwuaji. Lakini Makari alikataa akasema: “La, sitauliza jina la mwuaji. Inatosha kumwokoa mtu huyu aliyesingiziwa kwa uongo. Si kazi yangu kumtafuta mwuaji! Labda mwuaji mwenyewe amekwisha juta dhambi yake na anatubu ili roho yake ipate kupona!“

Siku moja Makari aliwasimulia watawa: “Nilipokuwa natembea jangwani, nilikuta fuvu la kichwa nchini. Nilipoligusa kwa fimbo langu fuvu ikaanza kuzungumza. Nililiuliza: ‘Wewe, ni nani?‘ Fuvu likanijibu: ‘Mimi nilikuwa kuhani mkuu wa miungu wa Wagiriki waliokuwa wakikaa mahali hapa. Lakini wewe ni Makari, pneumatophori, yaani, mbebaji Roho Mtakatifu. Wakati wowote unapowaombea wanaokaa matesoni wanajisikia raha zaidi kidogo.‘ Nikaliuliza: ‘Raha hiyo na mateso hayo ni raha na mateso gani?‘ Likanijibu: ‘Kama mbingu zimetengana na dunia, vivyo hivyo kuna chini yetu moto. Sisi tunakaa katikati ya moto kutoka miguuni hadi kichwani, lakini tunageuziana migongo, hatuonani ana kwa ana. Wakati unapotuombea, kila mmoja wetu anaweza kuona kidogo uso wa mwenzake. Ndiyo raha yetu.‘ Nikalia na kusema: ‘Ole siku mwanadamu alipozaliwa‘. Nikamwuliza tena: ‘Je, kuna mateso zaidi kuliko hayo?‘ Fuvu likanijibu: ‘Ndiyo, kuna adhabu kali zaidi chini yetu‘. Nikaliuliza: ‘Ni nani wanaokaa kule?‘ Fuvu likanijibu: ‘Sisi, kwa sababu hatukumjua Mungu tunahurumiwa kidogo, lakini hawa waliomjua Mungu na waliomkana wamo chini yetu‘. Basi nikachukua fuvu na kulizika.“

Siku moja mzushi wa kikundi cha Hieracites, wale wanaoafikiana na Wamanikeo, akafika katika jangwa la Shete, akiwa na nia ya kupotosha imani ya watawa, kwa maneno yake ya hila. Akawa na uhodari hata kumfikia Makari. Akajadiliana na Makari na ndugu, akiongea nao kwa upole na kuwaonyesha kwa kutumia Maandiko Matakatifu upotovu wa imani yao. Kulikuwa hatari kwa ndugu kutegwa na maneno yake ya hila. Kwa hiyo, Makari akiogopa kwamba watawa watayumba katika imani yao, akapendekeza kwamba kuliko *kushindana na maneno ambayo hayana faida, bali huwaharibu wasikiao*, afadhali *kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu*

kwa matendo.[3] Wakakubaliana waende katika shamba la wafu la watawa na yule atakayefufua mtu aliyezikwa atambulike kama Mwalimu wa kweli wa Mungu na wafuate imani yake. Wasikilizaji wote wakakubali. Mzushi akadai Makari aanze kwa sababu mapendekezo yalitoka kwake. Kwa hiyo walipofika katika shamba la wafu, Makari akapiga magoti, akainama kichwa chini na kukaa kimya kwa muda. Baadaye akainua macho yake mbinguni akasema: "Bwana, utuonyeshe, kati yetu wawili, nani anayeshika imani ya kweli, kwa kumfufua mfu huyu. "Ndipo akamwita kwa jina lake ndugu aliyezikwa karibuni. Huyu ndugu akaitika. Walipoondoa ardhi yote na kufungua kaburi lake walimkuta mzima. Wakamchukua na kumpeleka kwa abate Makari, kwa mshangao mkubwa wa yule Mzushi, ambaye alipoona jambo hilo alikimbia kwa mbio sana na kutoonekana tena mahali pale.

Lakini inafaa zaidi kuangalia fadhila zake. Utakatifu wake, uliosifiwa na vizazi vyote vifuatavyo, umejengwa juu ya msingi wa kweli, yaani kujitambua jinsi alivyo na kujikana, akionyesha unyenyekevu wa kweli. Jambo hilo linaonekana kwake kwa kuvumilia kwa furaha fedheha na kukimbia sifa. Wageni wa heshima walikuwa daima wale waliomtukana na kumdhihaki. Kwa hao alikuwa wazi, lakini kwa wale waliomfikia kusikiliza mambo ya Mungu na kumwonyesha dalili yoyote ya heshima na sifa alikaa kimya. Tabia hiyo ilijulikana na wengi, kwa hiyo waliomfikia kuongea naye mambo ya Mungu, daima walianza kumwambia matusi, dhihaki na fedheha waliosikia kuhusu yeye au kukumbusha aliyosema kuhusu madhambi yake ya ujana, wakiwa na uhakika kwamba watampendeza.

Shetani mwenyewe alikiri kwamba ndiyo unyenyekevu wake, na siyo majikatalio yake, ulikuwa unamfanya ashindwe. Siku moja Makari alitoka kwenye mabwawa alipotafuta makuti na matete. Akawa anarudi kijumbani kwake. Mara akakutana na Shetani aliyechukua mundu. Shetani akamwonyeshea mkono akataka kumpiga Makari kwa mundu akashindwa. Basi akamwambia Makari akasema: "Wewe Makari, unaniaibisha vibaya sana kila wakati nami ninashindwa kukulipiza kisasi. Mimi ninafanya yote unayofanya wewe. Wewe unafunga; nami ninafunga maana tangu nilipoumbwa sijala kitu. Wewe unakesha; nami tangu mwanzo wa dunia mpaka leo sijalala usingizi. Lakini unanipita kwa jambo moja!" Makari akamwuliza akasema: "Ninakupita kwa jambo gani?" Shetani akamjibu akasema: "Kwa unyenyekevu wako! Kwa sababu ya unyenyekevu wako ninashindwa kabisa siku zote kukudhuru rohoni mwako!" Shetani aliposema

[3] 2 Tim 2:14-15.

maneno haya Makari akainua mikono yake mbinguni kwa sala na Shetani akatoweka.
Unyenyekevu wake uliandamana na upole wake wa ajabu. Kwa kawaida fadhila hizo mbili zinaonekana kwa pamoja. Na upole wake uliwaongoa watu wengi zaidi kuliko miujiza iliyotendeka kwa mikono yake. Siku moja Makari alienda mpaka mlima Nitria. Alimwambia mwanafunzi wake kumtangulia kidogo. Baada ya kwenda mbele, mwanafunzi akakutana na mpagani kuhani, aliyekimbia kuelekea kwake, akibeba boriti zito sana. “Unakimbia wapi, wewe pepo mchafu?“ mwanafunzi akasema kwa sauti kubwa. Huyu kuhani akajisikia kwamba ametukanwa vibaya sana. Akasimama na kuanza kumpigapiga mwanafunzi mpaka kumwacha amejeruhiwa sana. Mbele kidogo kuhani akakutana na Makari.
“Nakutakia wema,  wewe unayehangaika kwa kubeba mzigo mzito, nakutakia wema!“ akasema abate Makari. Kuhani akashangaa na kumjibu:
“Unaona nini ndani yangu hata unanitakia wema?“
“Naona unahangaika, na pia unakimbia hujui wapi pa kwenda?“
“Kwa kweli, nimeguswa sana na salamu yako. Naona kwamba wewe ni mtumishi mkuu wa Mungu. Mtawa mwingine alinitukana aliponikuta, lakini nilimpatia aliyostahili.“
Na baadaye akashika miguu ya Makari akalia: “Sitakuacha mpaka utakaponifanya kuwa mtawa“.
Wakatembea pamoja hadi walipofika mahali mwanafunzi wa Makari alipolala. Hakuweza kutembea, kwa hiyo walimwinua na kumbeba kati yao wawili mpaka walipofika monasteri. Watawa walipomwona mpagani kuhani pamoja na Makari wakashangaa na wakafurahi kumpokea kama mtawa. Wapagani wengi wakaongoka kuwa Wakristo kwa sababu ya ushuhuda wake.
Makari akasema: “Maneno ya kiburi na machukizo yanaweza kuwafanya hata watu wema kutenda mabaya, lakini maneno ya unyenyekevu na upole yanaweza hata kuvuta watu wabaya kutenda mema. Akaendelea kuwaambia: “Tukikumbuka mabaya watu waliyotutendea, tunaacha kumkumbuka Mungu. Tukikumbuka mabaya pepo wanayotutendea, hapa kweli hatutashindwa hata mara moja!“ Tena alisema: “Unapomkosoa ndugu yako aliyezama katika dhambi na unaanza kukasirika, hapa unafuata tamaa yako; Usipoteze amani yako kwa ajili ya kumwokoa mwenzako“.
Unyenyekevu wa Makari uliandamana pia na hofu ya haki ya Mungu, ujuzi na kichomo cha dhambi zake, fadhila ambazo zilikuwepo hadi kufa kwake. Kuthibitisha jambo hilo inasimuliwa kwamba, kabla kidogo ya kufa kwake, watawa wa Nitria walimpasha habari kwamba wanataka afike kwao kupokea baraka zake kabla hajaenda kwa Bwana. Kama sivyo wote watafika kwake

kumtembelea. Akakubali kwenda. Alipofika na kuwaona watawa wote waliokusanyika na kutaka kusikiliza neno kutoka kwa Mungu kwa kinywa chake, kuliko kuwahubiria, alianza kulia machozi akisema: “Tulie, ndugu, tulie wakati tunapopata nafasi. Machozi yanayobubujika kutoka macho yetu yasafishe madoa ya madhambi yetu, kabla hatujaondoka kwenda ulimwengu mwingine, ambapo tukilia, machozi yatatusaidia tu kuongeza miali ya mateso yetu“. Machozi na maneno ya Makari yalifanya kwamba watu wote walilia na kujitupa chini ili kumwomba msaada wa sala zake.

Wakati mwingine mtawa mmoja alitaka kufundishwa na Makari namna ya kuhakikisha wokovu wake. “Kimbia“, alisema mtu wa Mungu, “kuhusiana na watu, na ukae katika kijumba chako, na humo ulilie madhambi yako, na kama malipizi bora ya madhambi yako, ujitahidi kutawala ulimi wako kwa kukaa kimya, na kutawala tumbo lako kwa kufunga“. Na kwa watawa wote alisema siku moja walipotoka kanisani: “Kimbieni, ndugu, kimbieni“. Mmoja akamwuliza: “Baba, tuende wapi mbali na ulimwengu kuliko kukaa katika jangwa hili?“ Makari aliweka kidole chake kinywani mwake na kusema: “Namaanisha tukimbie na jambo hilo“. Na bila kusema kitu tena akaingia kijumbani mwake na kukaa huko kimya.

Sala za Makari zilikuwa kwa namna nyingine bila kukoma. Ilisemekana kwamba karibu daima alikuwa katika hali ya jazba, yaani katika estazi, akichukuliwa nje ya mwili wake, na kwa muda mrefu kuongeana na Mungu kuliko kujishughulisha na mambo ya ki-dunia. Ili kukaa pamoja na Mungu katika sala, alichimba njia chini ya ardhi kwenda katika pango moja, mbali na mita kama 100. Mara nyingi alienda kule, mbali na watu, kukaa peke yake na Mungu wake, bila kusumbuliwa  na wageni waliokuwa wanafika wakivutwa na sifa zake. Kwa muda wa miaka mitano alikuwa anawaza kwenda mbali zaidi katika jangwa. Kwa kawaida yake kutotenda kwa haraka, akapima mawazo hayo ili yasije kuwa vishawishi. Lakini kwa sababu mawazo hayo yaliendelea alitambua kwamba ndiyo mwito kutoka kwa Mungu. Basi akaondoka kwenda ndani ya jangwa zaidi. Kule akakuta dimbwi la maji na ndani yake kisiwa kidogo walipoishi wakaa pweke wawili kwa muda wa miaka arobaini, mbali na mazungumzo na watu. Walifikia ukamilifu wa ajabu, hata Makari baada ya kuwaona na kuongea nao aliwaambia watawa wa Nitria baadaye: “Hakustahili kuitwa mmonaki, lakini aliwaona wamonaki wa kweli“. Fundisho alilopata kutoka kwao ni kwamba mtawa lazima aache yote ya ulimwengu, na ikiwa anajiona mdhaifu mno kuacha yote kama wamonaki hawa, afadhali aingie kijumbani mwake na kulilia madhambi yake.

Abate Makari alipokuwa anasali, akasikia sauti ikisema: “Bado hujafika utakatifu wa wanawake wawili wanaoishi katika mji wa karibu”. Basi,

akashika gongo lake na akaenda mjini kuwatafuta. Alipofika nyumbani mwao alipiga hodi, mwanamke mmoja akamkaribisha kwa furaha. Walipokusanyika wote watatu akawauliza: ”Nimehangaika sana kutoka jangwani hadi kufika kwenu ili nijifunze jinsi mnavyoishi. Natumaini kwamba mtanieleza yote.”
“Baba, usiku huu wote wawili tulikuwa kitandani pamoja na waume zetu. Unawezaje kujifunza kutoka kwetu?”
Lakini mzee Makari akaendelea kushikilia kuomba wamwambie siri ya maisha yao, namna yao ya kuishi kitakatifu.
“Sisi si ndugu”, wakasema, “lakini ikatokea kwamba tuliolewa na kaka wawili, na kwa miaka kumi na mitano tunaishi katika nyumba hii na hatujafarakana. Tunaishi pamoja kwa amani hadi leo. Tulikubaliana kwamba, ikiwa waume zetu watatuhusu, tutaingia katika konventi ya masista na kutunza ubikira wetu. Lakini waume zetu hawakuturuhusu, ingawa tuliwasihi sana. Kwa hiyo, tulimwahidi Mungu kwamba hatutazungumza kuhusu mambo ya dunia, neno lolote bure halitatoka kinywani mwetu, mpaka siku ya kifo chetu”.
Aliposikia hayo Abate Makari alisema: “Kwa kweli, siyo muhimu kuwa bikira, au kuolewa kama ninyi, au kuishi kama watawa wa kike au kuishi ulimwenguni. Mungu, anayewapa Roho Mtakatifu kwa wote, anataka nia njema” .
Wivu wake kufikia utakatifu wa juu ulimpeleka Makari kwenda safari ya siku kumi na tano kutoka jangwa la Shete hadi mlima alipoishi Mt. Antoni. Baada ya kukanyaga kwa siku nyingi mchanga wenye moto sana, alifika mahali pale, akapiga hodi mlangoni pa kijumba cha Antoni. Antoni akatoka nje na kumwuliza: “Wewe ni nani?“ Alipojibu kwamba yeye ni Makari, Antoni akaingia tena katika kijumba chake, akafunga mlango. Alitamani tangu siku nyingi kumwona Makari aliposikia utakatifu wake. Kwa hiyo aliamua kujaribu uvumilivu na unyenyekevu wake. Makari akabaki mlangoni mpaka Antoni alifikiri kwamba amemjaribu vya kutosha. Akamfungulia mlango na wakakumbatiana kwa upendo. Antoni akamkaribisha vizuri kadiri alivyoweza. Jioni akatayarisha makuti ili kutengeneza mikeka usiku. Makari, aliyependa kufanya kazi kwa mikono yake, na kuchukia kukaa bila kufanya kazi, alitaka kumsaidia Antoni. Kwa hiyo wakakaa kwa pamoja wakifanya kazi na kuongea mambo ya Mungu na kumsifu. Asubuhi yake Antoni alishangaa kuona kazi kubwa aliyofanya Makari. Basi akachukua mikono yake na kuibariki na kukiri kwamba fadhila nyingi zimo mikononi mwake. Sijui kama ni siku ile au wakati mwingine Antoni alimwona Roho Mtakatifu akimshukia Makari. Iliandikwa kwamba Antoni mwenyewe alisema kwamba alimwona Roho Mtakatifu akiwashukia watumishi watatu wa Mungu, ambao walionekana

wamejaa neema zake kwa namna ya ajabu, hawa ndio Mt. Atanasi, Mt. Pakomi na Mt. Makari.
Kuhusu majikatalio ya Mt. Makari na wafuasi wake wa jangwa la Shete, ni vema zaidi kuyastajaabia kuliko kuyaiga, hasa namna walivyofunga. Tunasoma mahali pengine kwamba ilikuwa desturi yake kula mara moja kwa wiki. Makari alimwambia mfuasi wake Evagrius, aliposhikwa na kiu ya ajabu, jua lilipowaka sana mchana, kwamba yeye kwa muda wa miaka ishirini, hakujitosheleza katika kula, kunywa au kulala. Kila wakati alijipimia uzito wa mkate atakaokula, au kiasi cha maji ya kunywa na daima aliegema ukutani kuliko kujilaza, alipoiba – kama alivyosema mwenyewe – usingizi mdogo mwili wake uliodai.
Inasemakana kwamba Makari alipokuwa anajipumzisha pamoja na watawa wenzake, alijiwekea sheria hii, “kama divai inapatikana, basi unywe kwa ajili ya ndugu zako, lakini kwa kila kikombe cha divai ulichokunywa, utabaki siku moja bila kunywa maji.“ Kwa hiyo, ndugu walikuwa wanamfurahisha kwa kumpatia divai. Lakini mfuasi wake alipopata habari hiyo akawaambia: “Kwa jina la Mungu wetu, usimpatie tena divai, au atakufa katika kijumba chake.“ Waliposikia hayo, wakaacha kumpatia divai.
Kama alivyojikatalia kikamilifu katika kula, kunywa na kulala, vivyo hivyo alitawala kabisa tamaa zake. Na alilotenda alilifundisha wafuasi wake watawa. Alikuwa anasema kwamba mtawa wa kweli ni yule ambaye anajikatalia katika kila kitu. Njia ya kuepuka mauti ya roho iliyoletwa na dhambi ni kupokea na kukubali madharau na sifa, umaskini na utajiri, njaa na utele wa chakula. Siku moja kijana akamwuliza ili ajue njia za kufikia ukamilifu. Akamtuma mahali ambapo kulikuwa na maiti nyingi. Akamwamuru kuwatukana matusi yote, tena kuwatupilia mawe, kujaribu kuwakasirisha. Kijana akafanya kama alivyoamuru. Aliporudi Makari akamwuliza jinsi maiti walivyopokea matusi hayo, na walisema nini. Kijana akamjibu: “Hawakusema neno lolote“. Kesho yake Makari akamtuma tena kijana na kumwamuru awasifu kwa maneno mazuri na matamu, na kuangalia jinsi watakavyojibu. Kijana akamjibu: “Hawakusema kitu“. Ndipo Makari akamwambia kijana kwamba ikiwa anataka kuwa mkamilifu inambidi kufuata mfano wao, kutokasirika au kuwa na uchungu moyoni mwake watu watakapomshutumu au kumdharau. Vivyo hivyo kutojivuna kama watu watakapomsifu, bali daima kumwangalia Yesu Kristo na kutafuta kumpendeza yeye tu.
Makari alipofika umri wa miaka sabini na sita, dhiki kubwa dhidi ya watawa wote ilitokea. Dhiki hiyo ilisababishwa na Lucius, mfuasi wa Ario, ambaye alinyang’anya Kiti cha kitume cha Aleksandria, baada ya kifo cha Mt. Atanasi, kwa msaada wa Kaizari Valens. Mtu huyu alipoona kwamba watawa

walimpinga mafundisho yake, na ya kwamba watu walishauriwa sana nao kushika imani ya Kanisa Katoliki, akaamuru jeshi la askari waende jangwani na kuwashurutisha watumishi hawa wa Mungu kukana dini yao. Wengi wa watawa wa Mlima Nitria waliuawa wakati ule, na wengine wengi, pamoja na maaskofu, mapadri na mashemasi, walihamishwa. Makari wa Misri, Makari wa Aleksandria, Isidori wa Shete na Pambo, abate mtakatifu wa Nitria, kwa amri ya Lucius, walikamatwa usiku na kuhamishwa katika kisiwa kimoja cha Misri, ambapo wapagani tu waliishi, ili wasiendelee kuwahudumia wakristo kama padri, wala kufarijiwa kwa jinsi yoyote na wakazi wa pale. Katika kisiwa kile kulikuwepo hekalu la Pepo, ambao wakazi wa kisiwa waliliheshimu sana. Lakini angalia ajabu ya Mungu! Mara moja, walipokanyaga nchi hiyo, pepo wote waliokaa hekaluni, wakafanya ghasia. Mmojawapo akampagaa binti wa kuhani wa hekalu, ambaye akaanza kupiga kelele, na kujitupa huko na huko. Watu wote wakafika kumwangalia. Binti huyo akakimbia kati ya watu, akianguka mara, na mara nyingine kujiviringisha chini, akitoa povu na kusaga meno. Na ghafla akainuliwa juu na kupelekwa mahali ambapo Watakatifu walipotua miguu yao. Watu wote walimfuata na kutazama yatakayotokea. Binti akaanguka miguuni mwa Makari na wenzake. Pepo akasema: “Ninyi watumishi wa Yesu Kristo, jinsi uwezo wenu ni mkubwa! Ninyi watumishi wa Mungu kwa nini mnafika hapa kutufukuza kutoka mahali ambapo tulitawala kwa muda mrefu? Hapa tulijificha baada ya kufukuzwa kutoka nchi, kwa sababu mlitufukuza kutoka miji na vijiji, milima na vilima, na hata mahali ambapo hakuna mtu aliyeishi kabla yenu. Tulitegemea kupumzika kidogo katika kisiwa hiki, kati ya vinamasi na mabuga. Mnakuja kutufukuza kutoka ngome yetu ya mwisho.“ Pepo alipozungumza hayo Watakatifu walitumia uwezo wao waliopewa na Bwana na kumwamuru Pepo kutoka kwa jina la Yesu, Mwana wa Mungu. Pepo akatii na kumwangusha binti chini; naye akawa kama amekufa. Watakatifu walimwombea na kumwinua kutoka chini, na kumpatia baba yake, yu mzima kabisa. Wakashika nafasi kuwahubiria watu habari ya Yesu, Mwokozi. Wote waliwasikiliza kwa makini baada ya kuyaona maajabu ya Mungu. Na Mungu akabariki maneno yaliyosemwa na Watumishi wake, hata kuhani, na binti yake na wengi kati ya watu, waliwaangukia miguuni mwao wakitaka kujua zaidi watakayopasa kutenda ili waokoke. Na watu wote wa kisiwa, kufuatana na mfano wao, wakaongoka. Wakashika imani yao kwa nguvu sana, wakabomoa hekalu lao waliloheshimu sana, na wakaanza kujenga kanisa. Wakafundishwa na kubatizwa. Kuhamishwa kwao kulisababisha baraka nyingi kwa watu hawa, na kueneza imani, ambayo kwa sababu hiyo,

walihamishwa. Waliposikia habari hizo, adui na watesaji wao, wakaamuru watumishi wa Mungu warudi mahali pao jangwani.
Makari aliishi miaka mingi baada ya dhiki hiyo. Alipofika umri wa miaka 90, miaka 60 jangwani, akaenda kwa furaha kukaa pamoja na Mungu wake, mnamo mwaka 390 au 391. Jina lake linakumbukwa katika kitabu cha watakatifu, *Roman Martyrology*, kwa tarehe 15 mwezi wa Januari.

# Sura ya 2
# Maisha ya Makari Mdogo

Makari Mdogo alizaliwa nyuma ya mwenzake. Makari Mdogo huyu alizaliwa katika mji wa Aleksandria mwaka kama 310 B.K. Kwa hivi watu wengine walimwita jina lake Makari wa Aleksandria au Makari mkaa mjini.
Alipokuwa kijana alijifunza kazi ya kuoka mikate. Aliishi kwa kuuza mikate mitamu, matunda na chakula kingine. Alipotimia umri wa miaka arobaini alikuwa mkatekumeni akapata ubatizo.
Baada ya ubatizo wake Makari akiitwa na Mungu kuishi maisha ya utakatifu, aliacha mambo ya dunia akaenda jangwani kujiweka chini ya Mt. Antoni, ili kujifunza sayansi ya kweli ya Watakatifu. Akajifunza kwa haraka sana, na muda si muda, akahitimu kuwa mwalimu wa watu kuwafundisha njia ya maisha ya kweli. Siku moja Antoni alipokuwa pamoja na Makari akamwomba makuti mazuri, ambayo Makari aliyaweka pembeni kwa kazi yake. Makari akamjibu: "*Usitamani mali ya jirani yako*". Mara makuti yakakauka na kunyauka kama yangaliunguliwa. Antoni alipoona jambo hilo akamwambia Makari: "Naona Roho Mtakatifu anakukalia rohoni mwako. Na tangu leo ujiangalie kama mrithi na mwandamizi wa neema na vipaji vyangu".
Makari akaenda. Baada ya muda Shetani alipomwona amechoka kwa safari yake jangwani na kukosa chakula akamshawishi akisema: "Ulirithi neema ya Antoni, kwa nini usiutumie uwezo huo na kumwomba Mungu, chakula na nguvu". Mtakatifu akamjibu: "Bwana ni nguvu yangu, Bwana ni utukufu wangu. Na wewe uondoke, usijaribu kumshawishi mmoja ambaye ana nia kuwa mtumishi wa Utukufu wa Mungu". Kwa maneno hayo Shetani akaondoka, lakini akachukua umbo la ngamia anayeonekana amepotea jangwani, akibeba aina mbalimbali za mahitaji ya maisha. Akasimama karibu na Mtakatifu. Makari akigundua hila ya Shetani akamwomba Mungu na mara njozi ikatoweka.
Makari huyu alikuwa na makao manne mbalimbali na anaonekana kuwa ametembea huko na huko kuwatazama wakaa pweke wenzake. Kijumba chake cha kwanza kilikuwa katika jangwa la Shete. Akajenga kijumba chake cha pili katika jangwa la Lybia, karibu ya mpaka. Amoni mtakatifu alipoanzisha utawa mahali palipoitwa Nitria, karibu ya Aleksandira, Makari alijijengea nyumba yake nyingine pale pale. Mwendo wa saa mbili kutoka Nitria ulikuwa mji wa watawa wakaa pweke wengine, mji huo wa wakaa pweke uliitwa Selia, maana yake mji wenye vijumba vya watawa, Makari akajenga kijumba kingine na

akapenda kuishi pale muda mrefu. Kwa sababu ya utakatifu wake akapadirishwa na kuwekwa kuyaangalia mahitaji ya watawa wote walioishi katika jangwa hilo. Hapa aling'aa kwa fadhila na miujiza ya ajabu, hata akaangaliwa na watu kama mwanga mkubwa wa Kanisa wakati wake. Kwa hiyo alishiriki pia katika mateso yaliyosababishwa na kaizari Valens, mfuasi wa Ario, wakati dhiki ilivuma hasa upande wake. Alihamishwa pamoja na Makari mwingine katika kisiwa kimoja cha Misri, kama ilivyoandikwa katika maisha ya Makari mkubwa.


Alitumia muda wake kusali mara mia kwa siku, na kufanya kazi ya mikono ili kujipatia mahitaji ya maisha yake. Na muda uliobaki aliutumia kwa ajili ya kuwashauri watawa na kuwafundisha. Na wakati huu majikatalio aliyokubali yalikuwa makubwa kiasi kwamba yanafaa kustajaabiwa kuliko kuigwa. Kufunga kwake kulidumu muda mrefu. Makari alikuwa na bidii sana kufuata mifano bora ya watawa wenzake. Alipata habari kwamba watawa wa baba Pakomi hawali chakula kilichoandaliwa kwa moto wakati wa Kwaresima. Akanuia kutenda vile vile. Muda wa miaka saba akatumia mboga mbichi au mboga iliyolowekwa basi. Lakini hakuridhika ugumu huu kwa kuwa alisikia kwamba mtawa mwingine ya baba Pakomi kwa siku moja hula ratili moja tu ya mkate, yaani wakia kumi na sita. Basi Makari akajitahidi kumshinda. Akachukua chombo kilichofanana na mtungi chenye mdomo mdogo sana. Akakijaza maji akatwa mkate akauvunjavunja. Akaviloweka vipande vya mkate katika mtungu ule wa maji. Akakusudia kula mkate kwa kadiri anavyoweza kutoa kwa mkono mmoja katika mtungi ule. Mwenyewe aliwasimulia wenzake kwa furaha ilivyokuwa, akasema: "Mkono wangu kila mara ulishika vipande kadha wa kadha ndani ya mtungi. Lakini nikirudisha mkono ilinipasa kunyosha vidole, nisifumbe mkono, maana mdomo wa mtungi ulikuwa mdogo mno na hivi vipande vingine vimeshindwa kupita vikarudi katika mtungi.“ Kwa njia hii hakuweza kula mkate zaidi ya wakia nne au tano. Akajisumbua hivi kwa njaa muda wa miaka mitatu.

Makari mtakatifu akakusudia kushinda usingizi. Mwenyewe alisimulia mashindano haya akasema: "Siku ishirini kutwa kucha sikuingia kijumbani kwangu. Nikasumbuka mchana kwa joto la jua, na usiku nalitaabika kwa baridi. Hivi nimejishinda nisipate kushindwa kwa usingizi. Baadaye nimekubali kulala usingizi muda mfupi ili niitike mahitaji ya ubinadamu wangu.“

Wakati mwingine Makari alitaka kusali siku tano kutwa kucha akimwelekea Mungu kwa mawazo yake yote. Akaingia katika chumba chake cha ndani akafunga mlango, ili asifikiwe na mtu. Akaanza sala yake akasema: "Wewe roho yangu, angalia sana usishuke kutoka mbinguni. Utawakuta huko Malaika

na Malaika wakuu, pia Makerubimi na Maserafimi na Mungu mwenyewe aliyewaumba wote. Ushinde huko, usishuke wala usishike mawazo ya kidunia.“ Akamwelekea Mungu kwa mawazo yake yote siku mbili kutwa kucha. Lakini hapa Shetani alimghadhibikia kabisa akatokea kama moto unaounguza vitu vyote vya nyumbani kwake. Hata mkeka aliousimamia ulionekana kama unaungua moto, ikiwa kama Makari mwenyewe ataungua. Lakini Makari hakuangalia udanganyifu huu wa Shetani, bali alimwelekea Mungu tu. Siku ya tatu akaingiwa na hofu na mawazo yake yakatawanyika sana kwa sababu ya kuogopa. Akaacha kuendelea kwa sala yake. Akatambua kwamba Mungu mwenyewe alitaka hivi, asipate kujivuna kwa ajili ya sala yake.

Wakati mwingine asubuhi mapema Makari alikuwa anakaa katika kijumba chake, mbu akatua juu ya mguu wake na kumwuma. Aliposikia maumivu akamminya kati ya vidole vyake, mara mkono wake ukachafuka damu. Akajihukumu na kukusudia kujilipizia kisasi kwa mwili wake. Akaenda upwekeni kwenye mabwawa. Akakaa kule katika matope yale miezi sita. Katika vijiti vya mabwawa yale walikuwako inzi wakubwa na wakali waliofanana na manyigu. Akakubali wamuume katika mwili wote ili maumivu yao yapoze moto wa vishawishi vyake. Baada ya miezi sita, aliporudi kijunbani kwake alifanana na mtu mwenye matende. Watawa wenzake hawakumtambua tena kwa sura yake, bali walimjua kwa sauti yake tu. Katika upweke wake Makari alisikia sifa njema za baba Pakomi na za wanafunzi wake waliokaa katika utawa wao wa Tabena katika jangwa la Teba.




Akatamani sana kuona mwenendo wao bora, ingawa ilikuwa safari ya siku kumi na nne mpaka Tabena. Basi Makari akaacha mavazi yake ya mkaa pweke akavaa kama mtu anayetafuta kazi ya kibarua. Akaenda kwenye utawa wa Pakomi mtakatifu asiogope taabu za safari ya jangwani.

Alipofika pale aliomba kuonana na mkubwa wa watawa. Pakomi mtakatifu akatokea mlangoni na Makari akajisingizia kuwa mtu wa bure. Akamwomba baba Pakomi akasema: “Ninakuomba unipokee katika utawa wako, maana nataka kuwa mtawa!“ Pakomi mtakatifu akamjibu akasema: “Wewe huwezi kuwa mtawa, maana u mzee. Utashindwa kushiriki kazi zote za watawa. Hata wengine walioingia utawa walipokuwa vijana wanasumbuka sana kutimiza

lazima zao. Lakini wewe mzee utashindwa kabisa kwa majaribu yatakayokupata katika utawa. Halafu utakasirikia ugumu wa utawa mpaka utaanza kututukana na kuacha kazi hii kwa moyo wenye uchungu.“ Basi baba Pakomi akakataa kumpokea Makari miongoni mwa wanafunzi wake akamwacha penye mlango akaingia nyumbani. Makari akashinda pale mlangoni siku saba kutwa kucha kwa uthabiti, asile chakula wala asinywe maji. Siku ya nane aliomba kuonana tena na baba Pakomi akamwambia: “Baba, unipokee katika utawa wako. Ukiniona kuwa nitashindwa kufunga au sitatimiza lazima zangu kama watawa wengine, basi utanitupa nje nami nitaridhika.“

Pakomi mtakatifu akalegea akampokea nyumbani kwake. Wakati ule watawa elfu moja na mia nne walikaa katika utawa ule alioingia Makari.

Zikapita siku chache tu ulipoanza wakati wa Kwaresima. Makari akaona jinsi kila mtawa alivyoanza kushika mwenendo wa pekee kwa kujisumbua wakati huu wa kutubu. Watawa kadha wa kadha waliacha kula mchana wote wakala usiku chakula kidogo tu. Watawa wa kundi jingine walikula kila siku ya pili tu na wengine walifunga siku nne kamili wakala chakula kidogo kila siku ya tano. Makari aliwaona watawa wengine walioketi chini walipofanya kazi kwa mikono wakati wa mchana, lakini usiku walikuwa wanasimama kiwimawima mpaka kucha.

Basi Makari akachukua makuti ya kutosha akayaloweka. Akaenda nayo mafichoni akasimama wima pale pale siku zote za Kwaresima. Hakula mkate wala hakunywa maji. Ingawa alikuwa amechoka sana hakupiga magoti kwa kupumzika hata kidogo, wala hakuketi chini wala kulala chini. Lakini kila Dominika alikula mboga mbichi majani kadha wa kadha ili ajisingizie kuwa anakula. Ikimpasa kabisa kutoka mafichoni kwake alitoka, lakini upesi sana alirudi pale pale. Akafanya kazi bila kufumbua kinywa chake, akasali kimya. Akanyamaza daima akasuka mikeka midogo.

Watawa wenyeji wengine waliokuwa wakinung’unika walipotambua kwamba mwanafunzi mzee yule amewapita wote walianza kufanya kelele mbele ya wakubwa wa utawa wakasema: “Mmekwenda kumchukua wapi mtu huyu anayeonekana kuwa hana mwili? Mbona anatuaibisha sisi sote! Mfukuzeni mtu huyu, au sisi tutatoka!“

Baba Pakomi akapata habari ya kelele za watawa wale akaanza kupeleleza desturi za Makari. Baadaye akamwomba Bwana amfumbulie hali ya mwanafunzi yule mzee. Akaonyeshwa katika sala kuwa mwanafunzi mzee ni Makari mtakatifu. Basi baba Pakomi akamwendea mafichoni kwake akamshika mkono akaenda naye kanisani walipokusanyika watawa. Wote wawili wakasimama mbele ya altare. Akambumbatia Makari aksema:

“Salamu, baba mheshimiwa! Wewe ni Makari ukanificha jina lako! Tangu miaka mingi nimesikia sifa zako njema nikatamani kuonana nawe. Ninakushukuru sana kwa sababu umewashinda wanafunzi wangu wasije wakajivuna kwa ajili ya matendo yao. Lakini ninakuomba sasa urudi kijumbani kwako. Tumefurahi mafundisho yako uliyotufundisha. Utuombee siku zote kwa sala zako!“ Basi Makari akatoka akarudi kwake.
Makari, licha ya majikatalio yake, alitawaliwa na upendo. Siku moja ndugu fulani akamletea zabibu wakati alikuwa na hamu kubwa kuionja. Lakini, kwa kujikatalia na kwa kuonyesha upendo, aliitumia mkaa pweke mwingine aliyekuwa mgonjwa na aliyeihitaji zaidi kuliko yeye. Mtu huyu mwema, baada ya kumshukuru kwa zawadi yake, kwa njia ya roho ile ya kujikatalia, na kwa upendo mkubwa, aliitumia mkaa pweke mwingine aliyeishi mbali kidogo. Yule wa tatu akaitumia kwa mkaa pweke wa nne. Na vivyo hivyo zabibu ikapita kwa mikono ya wakaa pweke wengi, hata wa mwisho, bila kujua zabibu ilitoka kwa nani, akampelekea kwa Makari. Mtakatifu akiitazama na kuitambua kwamba ni zabibu ile ile, na baada ya kupeleleza imepita kwa watu wengapi, alimshukuru Mungu kwa ajili ya roho ya kujikatalia watawa walionyesha wakati ule. Kwa sababu hiyo Makari akazidi kujikatalia na hakula zabibu.
Wakati mwingine Makari alikwenda kutembea kwa kuwa alitaka kuwatazama wakaa pweke wenzake. Aliporudi kijumbani kwake alimkuta mwizi mle mle. Mwizi alikwisha vunja malango akachukua vitu vyote alivyoona akavipakia punda aliyengoja nje;. Basi Makari akajisingizia kuwa msafiri anayepita njia. Akaingia kijumbani kwake akamsaidia mwizi kuchukua vitu vyake na kumtwisha punda. Walipotoa vitu vyake vyote na kufunga vizuri juu ya punda, Makari alimwaga mwizi wake akamhimiza akasema: “Kwa heri, mwenzangu! Kimbia upesi, maana mwenye nyumba yu karibu!“ Mwizi akatoka kwa haraka sana naye Makari akaingia kijumbani akasema: “Sikuchukua kitu nilipofika hapa duniani, bali nalitoka uchi tumboni mwa mama yangu. Bwana alinipa vitu hivi naye Bwana amevichukua. Imekuwa kama ilivyompendeza Bwana. Jina la Bwana litukuzwe daima!“
Makari alikuwa amejaliwa na Mungu kuwaponya wagonjwa na kuwafukuza pepo. Palladius anatusimulia kwamba aliwaponya watu wengi waliokuwa wamepagawa, idadi isiyoweza kuhesabiwa. Mbele ya macho yake, wakamleta kijana aliyepagawa. Makari akaweka mkono wake mmoja juu ya kichwa chake na mwingine kifuani mwake. Akasali sana hata kijana akaanza kuelea angani. Baadaye mwili wake ukavimba kama kiriba na kutunga usaha hadi akawa bonge ya erisipela. Alipopiga kelele maji yakatoka kwa njia ya milango yote ya mwili, na kurudi katika hali yake ya kawaida. Basi akampaka mafuta

na kumrudisha kwa baba yake. Akamwagia maji na kumwamuru asile nyama wala kunywa divai kwa siku arobaini. Akawa mzima kabisa.
Palladius alipokuwa pamoja naye walimletea msichana wa ukoo bora kutoka Thesalonike, aliyekuwa amepooza tangu miaka mingi. Akachua mwili wake na mafuta kwa mikono yake, kwa muda wa siku ishirini. Na wakati wote alikuwa anamwombea. Akamrudisha katika mji wake mzima. Baadaye alimtumia zawadi nyingi.
Ilisemekana kwamba binti wa baba wa nyumba akabadilishwa kwa njia ya uchawi wa mganga kuwa punda. Jamaa na ndugu zake walimwona kuwa punda na siyo tena binti yao mdogo mpendwa. Basi wazazi wake wakamleta kwa mzee Makari. Akawauliza: “Unataka nini?” Wakamjibu: “Punda huyu unayemwona , ndiyo msichana mdogo, binti yetu bikira, lakini watu wabaya walimbadilisha kwa nguvu zao za uchawi kuwa mnyama unayemwona mbele yako. Tunakuomba umwombe Bwana ili amrudishe katika hali ya zamani.” “Ninayoona mimi ni msichana mdogo mnayenionyesha” akamjibu, “sioni kitu chochote cha mnyama ndani yake. Mnayoniambia hayapo katika mwili wake, bali katika macho ya wale wanaomtazama. Ni njozi isababishwayo na pepo, siyo mambo ya kweli”. Akawachukua , binti na wazazi wake, katika chumba chake na akipiga magoti akaanza kumwomba Bwana. Akawalazimisha wazazi kuomba pamoja naye. Baadaye akampaka mafuta kwa jina la Bwana. Ndipo kazi ya pepo ikabomolewa, na wote wakamwona binti kama msichana mdogo.[4]
Siku moja watu walimleta padre fulani mgonjwa wakamlaza kwenye mlango wa kijumba chake. Padre huyu alikuwa na ugonjwa mbaya sana. Uso wake ulikuwa umeoza upande mmoja, hata mfupa ulionekana. Lakini Makari hakumwombea, wala hakumtazama wala hakumwambia neno. Kwa hivi padre alilala kwenye mlango muda mrefu. Basi akafika Palladius, (wakati ule alikuwa mfuasi wake), akamwomba Makari amhurumie mgonjwa. Lakini Makari akamjibu akasema: “Padre huyu hastahili kupona. Bwana mwenyewe amempa ugonjwa huu adhabu ya dhambi zake. Ukitaka apone, yafaa umshauri kwamba asisome tena misa tangu siku ya leo. Padre huyu alisoma misa baada ya kutenda dhambi ya mauti asitubu kwanza. Kwa sababu hii Bwana amempiga kwa ugonjwa huu!“ Basi padre mgonjwa akaahidi kwa kiapo kwamba ataacha kutimiza utumishi wa upadre, akakusudia kuacha kutenda dhambi. Basi Makari akaweka mikono kichwani kwa mgonjwa akamwombea. Baada ya siku chache padre akawa amepona akatimiza ahadi yake.

---

[4] De Vitis Patrum, book II, chapter XXVIII.

Kwa kuwa Makari aliwaponya wagonjwa wengi sana, Shetani alimtia mawazo ya kujivuna. Akamshauri atoke jangwani na aende kukaa mji wa Roma kwenye wagonjwa wengi zaidi watakaopona kwa sala zake. Makari akakataa mawazo haya, lakini yalimfikia tena na tena. Siku moja alisumbuliwa sana kwa mawazo ya namna hii. Basi Makari akafungua mlango wa kijumba chake akajitupa chini pale pale. Miguu yake ilikuwa nje, yeye mwenyewe ndani ya kijumba chake.Akawa amelala hivi akasema kwa sauti kubwa: "Enyi pepo, mnivute nje mkiweza. Mimi mwenyewe sitakwenda hata hatua moja ingawa inanipasa kulala hapa mpaka jioni!" Baada ya muda mrefu kishawishi kilikwisha naye Makari akasimama. Lakini jioni yake mawazo yake ya kujivuna yakamrudia tena. Basi Makari akachukua kikapu akakijaza mchanga. Akajitwisha mzigo mzito huu akaenda kutembea nao jangwani muda wa siku nyingi mpaka aliposhinda mawazo yake ya majivuno.
Siku moja alipokuwa akitembea na kikapu cha mchanga alikutana na Theosebius, kwa jina lingine Cosmetor, aliyetoka mji wa Antiokia. Theosebius akamwambia Makari akasema: "Baba, umechukua nini katika kikapu? Ninaomba kupokea mzigo wako usije ukasumbuka hivi." Lakini Makari akamjibu akasema: "Siwezi kuacha mzigo wangu, la! Maana ninausumbua mwili wangu uliotaka kunisumbua mimi. Kwa kuwa ni mzembe na mvivu alinishauri niende kutembea katika miji mikuu. Basi nikaona yafaa zaidi niutembeze jangwani humu!"
Alipokwisha tembea hivi muda wa siku nyingi alirudi pangoni kwake akawa dhaifu sana, lakini mawazo yale ya kujivuna yalikuwa yamekwisha kabisa.
Siku nyingine, wakati wa usiku, Shetani akagonga mlangoni mwake na kumwita: "Makari amka ili uweze kwenda kusali pamoja na watawa wengine wakati wa ibada ya usiku." Mtakatifu akijua, kwa mwanga wa Mungu, kwamba alikuwa Shetani, akamjibu: "Inakuhusu nini, wewe adui wa kweli yote, watawa wakienda kusali usiku?" Shetani akasema: "Nakuhakikisha Makari kwamba watawa hawakusanyiki kusali bila sisi kuwepo. Njoo uone kazi zetu." Basi Makari akamwomba Mungu kujua kama maneno ya Shetani yalikuwa kweli au sivyo. Akaenda mahali watawa walikusanyika kwa kusali. Akawakuta wakiitikiana zaburi. Akaona pepo, wenye umbo la wabilikimo weusi, wakiruka huko na huko kanisani, wakiwachezea watawa shere, wakiwavuruga mawazo, au wakiwalemesha na usingizi. Na baada ya kusoma zaburi kumi na mbili wakasujudu katika ukimya wa sala. Makari akawaona pepo wakijionyesha kwa mtawa mmoja kwa umbo la mwanamke, kwa mwingine kuonyesha jengo, mwingine safari, na kwa wengine kwa njia ya picha mbalimbali. Watawa wengine waliwafukuza kwa nguvu hata wakaanguka chini, lakini wengine waliwaruhusu kucheza kichwani na

mabegani mwao na kuwadharau. Makari akahuzunika sana kwa kuona mambo hayo. Akamwomba Mungu awaweke watawa wake huru na hila za yule Mwovu, akitumia maneno ya Zaburi: "*Mungu huondoka, adui zake wakatawanyika, nao wamchukiao huukimbia uso wake*", Zab 68:1. Baada ya kumaliza sala, Makari akawaita watawa, na akamwuliza kila mmoja. Akatambua kwamba walitawanyika mawazo yao, au kwa kujivuna, au kwa kutembea mbali kwa mawazo. Basi wakaelewa kwamba mawazo hayo yalisababishwa na pepo. Na njia ya kweli kuyaepa ni kujikinga wakati wa sala kwa kuunganisha roho zao na Mungu kwa kutumia nguvu zao zote.
Aliona jambo la kutisha sana ndugu walipopokea komunio. Waliponyosha mikono ili kupokea Ekaristi, pepo wengi waliruka kuweka makaa ya moto mikononi mwa wengine. Kwa sababu hiyo Mwili wa Kristo uliowekwa wazi mikononi mwao, kwa mikono ya mapadri, ulirudi altareni. Kinyume cha jambo hilo, pepo walirudi nyuma na kukimbia kwa hofu kubwa mbali na ndugu wengine, kama hao wamesaidiwa na nguvu kutoka juu. Aliona pia malaika wa Bwana aliyehudumia altareni, akibatilisha mikono ya mapadri iwe mikono yake. Na neema hiyo ilibaki daima naye. Kwa hiyo, alijua wazi mawazo pepo aliyaweka moyoni mwa mtawa alipoimba zaburi na kusali wakati wa kukesha; alijua pia wale wasiostahili na wale waliostahili kupokea Mwili na Damu ya Yesu.
Pia kwa neema ya Mungu alitambua kwamba wakati alipowagawia watawa komunio, siyo yeye aliyempatia komunio ndugu Marko mwasketi, bali malaika aliyempatia. Alikuwa anaona tu konzi ya mkono wake. Na huyu Marko mwasketi alikuwa kijana, aliyekariri kwa kichwa Agano la Kale na Agano jipya, akipita watawa wote wengine kwa upole na kutawala tamaa zake za mwili.
Mbali sana ya makao ya Makari mtakatifu lilikuwako kaburi la Jannes na Jambres, ambalo lilikuwa mali ya waganga wakubwa wa zamani waliokuwa na nguvu sana kwa Farao. Kaburi hili lilijengwa kwa mfano wa jumba kubwa katikati ya bustani yenye miti ya kila namna, na mitende na minazi. Makari alisikia kwamba katika jumba hili la kaburi wamekaa pepo wengi sana. Kwa hivi alitaka kuliona kaburi lile apate nafasi ya kuwapiga. Akaanza safari bila kujua njia. Kwa sababu hii alipita kati ya jangwa akifuata njia ya nyota kama watu wanaosafiri baharini na wanaofuata njia wanayoonyeshwa kwa dira. Akachukua matete mengi sana kadiri alivyoweza kuchukua. Kila mara akiisha tembea hatua elfu mbili alisimika tete katika mchanga, ili ayafuate wakati wa kurudi. Jioni ya siku ya tisa ya safari yake alifika karibu ya kaburi la waganga wale akalala usingizi muda mfupi. Kumbe Shetani alikuwa amemfuata akatoa matete yote aliyosimika Makari njiani. Shetani akayaweka matete yote penye

kichwa cha Makari wakati alipolala usingizi, akatoka. Makari alipoamka akayaona. Akatambua kwamba Mungu hakukataa tendo hili la Shetani Makari apate kujaribiwa. Maana alitumaini matete mahali pa kumtumainia Mungu aliyewaongoza Waisraeli jangwani kwa nguzo ya moshi (Kut 13:21/Kum 1:33).
Makari alipokaribia kaburi la waganga wa zamani alikutana na pepo sabini. Wakapiga kelele na walirukaruka. Wengine walitoa meno kama wanataka kumtafuna. Wakalia kwa sauti kubwa wakasema: "Makari, wewe kishawishi cha watawa, unataka nini? Ama tumewasumbua watawa wako? Hatuna shirika na wewe. Kwa sababu gani unatuudhi hapa nyumbani kwetu? Ukiwa mkaa pweke uridhike kukaa upwekeni. Huwezi kukaa hapa. Ondoka! Urudi kwako!" Wakazidi kupiga kelele na kumtukana Makari. Huyu akawaambia akasema: "Nataka kutazama kaburi la waganga hawa wa zamani waliokuwa wanafunzi wenu. Baadaye nitarudi kwangu." Alipokwisha ingia bustanini alikutana na pepo mwingine aliyeshika upanga wa moto na alitaka kumpiga Makari. Makari akamwambia: "Unanijia kwa upanga wa moto. Lakini mimi ninakujia kwa jina la Mungu wa Waisraeli aliye Bwana wa majeshi ya malaika wa mbinguni!" Papo hapo pepo akatoweka. Makari akatazama mimea yote ya bustani akaingia nyumbani walimozikwa waganga wale akachungua vitu vyote alivyoona. Baadaye akatoka tena bila hofu akarudi upwekeni kwake. Wakati aliporudi msurufu yake, yaani mkate na maji yalimwishia njiani. Akawa amedhoofika sana kwa njaa na kwa kiu na karibu alianguka chini kwa udhaifu wake. Basi Makari akaketi chini kwenye mchanga akapumzika. Pale pale ilikuwa kama anaona msichana mwenye kuvaa nguo nyeupe kabisa naye akachukua mtungi uliojaa maji, hata maji yalifurika. Mtoto akamwita Makari mara kwa mara aje kunywa maji. Ingawa mtoto hakusimama mbali zaidi ila kama hatua mia moja tu, Makari alishindwa kumkaribia. Udhaifu wake uliendelea hivi muda wa siku tatu na wakati huu wote alimwona msichana na mtungi wake uliojaa maji. Ndivyo kiu yake ilivyoongezeka na alikuwa amekauka kabisa kinywani. Kumbe msichana yule mwenye mtungi wa maji alikuwa udanganyifu tu wa adui wa wanadamu.
Basi Makari alipokuwa akitaabika kabisa kwa kiu yake Bwana alituma kundi la swala kumsaidia. Wanyama hawa walikuwa wameenea sana upande ule wa jangwa. Swala hawa wakapita karibu ya Makari. Mara swala jike mwenye ndama alisimama karibu ya Makari. Viwele vyake vilijaa maziwa hata vilidondoka maziwa. Makari akasikia sauti kutoka juu iliyosema: "Makari, nenda na unywe maziwa!" Makari akamkaribia swala jike akanywa maziwa akashiba. Bwana akamjalia tena makubwa zaidi. Akamwamuru swala yule kufuatana na Makari mpaka alipofika kijumbani kwake. Njiani kote swala

alimnyima mtoto wake maziwa akamnyonyesha mtumishi wa Mungu. Siku ya ishirini ya safari yake alifika kwenye kijumba chake.
Wakati mwingine Makari alitaka kuchimba kisima cha maji karibu ya makao yake. Wakaa pweke waliomfikia kumtazama walisumbuka kuchukua maji kutoka mbali. Akafyeka vichaka kwa nguvu zake zote. Mara nyoka mkali sana alimrukia akamng'ata. Makari akamshika kwa mikono yake midomoni kampasua mpaka mkiani kwake akasema: "Kwa sababu gani umeniuma bila kutumwa na Mungu?" akamtupa mbali akaendelea kufanya kazi yake.
Siku nyingine Makari aliketi katika chumba chake cha kwanza. Akafikiwa na fisi aliyechukua mtoto wake midomoni. Fisi akagonga mlango wa Makari kwa kichwa chake. Alipofunguliwa mlango akamtua mtoto wake penye miguu ya Makari. Mtoto wa fisi alikuwa amepofuka macho. Basi Makari akamshika mtoto wa fisi akamtemea mate machoni pake akasali. Pale pale fisi mdogo akapona akaona. Basi mtoto wa fisi akanyonya maziwa, kisha wote wawili wakatoka.
Siku ya pili fisi yule akamrudia Makari akamletea ngozi ya kondoo mkubwa. Makari akamwambia: "Umepata wapi ngozi hii? Haikosi umeiba kondoo kwa watu ukamtafuna. Lakini sitaki kupokea kitu kilichoibiwa." Fisi akashika tena ngozi kwa meno yake akainama kichwa akapiga magoti mbele ya Makari akaiweka chini mara ya pili. Makari akamwambia tena akasema: "Nimekwisha kuambia kwamba sitapokea zawadi yako isipokuwa uniahidi kwamba utaacha kuiba mali ya watu fukara!" Hapo fisi akaitika akainama kichwa. Basi Makari akapokea zawadi ya fisi mwenye shukrani.
Wakati Makari alipokaa katika jangwa la Shete, siku moja alisimama mbele ya nyumba yake. Akamwona Shetani anakuja na anapita karibu ya nyumba yake. Shetani alikuwa na sura ya mwanadamu na alikuwa amevaa kanzu iliyotumiwa siku nyingi sana, maana imetoboka huko na huko. Ndani ya kanzu Shetani alichukua chupa ndogo ndogo nyingi sana alizofunga kwa kamba. Makari akaziona kwa sababu ya matundu katika kanzu ya Shetani. Basi mkaa pweke mzee akamwuliza adui wa wandamu akasema: "Ati, bwana, unakwenda wapi?" Shetani akaitika akasema: "Ninakwenda kuwachungulia watawa wanaokaa bondeni huko!" Makari akamwuliza mara ya pili akasema: "Chupa hizi ulizochukua katika kanzu yako zina maana gani?" Shetani akamjibu akasema: "Chupa hizi zimejaa peremende ndogo zenye kunoga na jinsi wanavyopenda watawa!" Makari akauliza tena akasema: "Basi chupa hizo zote zimejaa peremende tu?" Shetani akasema: "Nidyo, lakini kila chupa ina namna yake mbalimbali. Watawa wakikataa ya namna moja ninawaonyesha namna ya pili, hata ya tatu na ya nne. Hivyo kila mmoja anapata namna ile anayofurahi mwenyewe."

Basi Shetani akaondoka akawaendea watawa waliokaa bondeni. Makari akaanza kusali. Akangoja pale pale mpaka adui yule wa wanadamu aliporudi. Basi Shetani alipofika tena kutoka bondeni Makari alimlaki kipande kidogo akasema: “Jambo, bwana, una habari nzuri gani?“ Shetani akasema: “Nitawezaje kuwa na habari nzuri?“ Makari akauliza: “Kwa sababu gani?“ Shetani akajibu: “Kwa sababu watawa wote wanaokaa bondeni huko ni watakatifu. Wote wamenidhaurau. Hawapendi, kusema nami hata neno moja!“ Makari akauliza: “Basi, ikiwa hivi watawa wale wote si marafiki zako!“ Ibilisi akamjibu akasema: “Yuko mmoja tu aliye rafiki yangu. Ah! Huyu ananisikiliza sana. Akiniona tu, basi anarukaruka kwa furaha!“ Makari akapeleleza akauliza: “Rafiki yako huyu ni nani?“ Shetani akajibu: “Jina lake Teokitisto!“ Basi Shetani akapita akatoweka.

Makari akashika njia ya kuwaendea watawa wale wa bondeni. Walipomwaona Makari kwa mbali walishika matawi ya mitende wakaenda kumlaki kwa shangwe. Kila mmoja alikuwa ameweka tayari kijumba chake kwa kuwa hawakujua atamfikia nani. Makari akamwita Teokitisto akaenda naye katika kijumba chake wakaongea kwa siri.

Makari akamwuliza: “Una habari gani, kaka?“ Teokitisto akajibu: “Nzuri sana, baba mheshimiwa!“ Makari akaendelea: “Siku hizi hukuona mawzao mabaya yanayokusumbua?“ Mwenzake akakataa kwa uongo akasema: “La, ila ninaona raha sana siku hizi, baba yangu!“ Basi Makari akamwambia akasema: “Tazama, kaka, tangu miaka mingi sana nimeshika mwenendo wa kitawa na watawa wote wananiheshimu. Lakini hata sasa ninapokuwa mzee ninasumbuliwa na vishawishi vibaya vya mwili.“ Teokitisto akamjibu akasema: “Baba, pia mimi ninashawishiwa sana kwa mambo haya!“ Makari akaendelea kujisingizia masumbuko mengine ya roho ili mwenzake asipate kuficha makosa yake. Baadaye akamwuliza akasema: “Unafunga namna gani, kaka?“ Theokitisto akamwambia kwamba siku zote anafunga mpaka saa tisa. Makari akasema: “Funga mpaka mwanzo wa usiku. Soma vitabu vya Injili mpaka utazijua kwa akili. Usome vile vile vitabu vingine vya Maandiko matakatifu. Ukitambua kwamba wazo baya linatokea moyoni mwako, usikaze macho yako chini, bali uyaelekeze juu mbinguni, maana hapa Mungu atakusaidia upesi sana.“

Ndivyo Makari alivyofundisha mtawa mwenzake. Basi akarudi upwekeni kwake. Zikapita siku chache. Makari alikuwa anajiburudisha tena kidogo mbele ya kijumba chake alipomwona Shetani yule mwenye chupa za peremende anakuja na anataka kupita. Makari akamwuliza: “Unakwenda wapi?“ Shetani akamjibu kwamba anakwenda kuwatazama watawa wa bondeni, akapita. Wakati aliporudi Makari alikuwa anamngoja akamwuliza:

“Habari gani za watawa wa bondeni?“ Shetani akamjibu akasema: “Habari ni mbaya tu!“ Makari akazidi kuuliza: “Mbaya namna gani?“ Shetani akamjibu kwa uchungu akasema: “Sasa watawa wote ni watakatifu. Lakini nimesikitika tena zaidi kwa kuwa rafiki yangu yule hanisililizi tena hata kwa neno moja. Sijui ameongoka kwa njia gani. Amenikatalia kabisa na utakatifu wake unapita ule wa wenzake wote. Basi, nikamwapiza nikamwambia kwamba siku nyingi sana zitapita mpaka nitakapokwenda kumtazama.“ Basi Shetani akatoka na Makari akaingia kijumbani kwake akamwabudu Mkombozi wa shukrani kwa sababu amemsaidia Teokitisto.
Siku nyingine Makari alisafiri jangwani. Jua lilipotua Makari alifika kwenye kaburi la wapagani wa zamani za kale. Kaburi hili lilifanana na jumba kubwa. Makari akaingia akataka kulala usingizi. Kwa kuwa hakuchukua mto wa kuweka kichwani alitoa maiti iliyokauka mahali pake. Akajilaza chini akatumia maiti ile kama mto alipoweka kichwa akalala usingizi. Basi pepo wakamwonea wivu kwa sababu hakuwa na hofu ya kulala juu ya maiti wakataka kumwogofya. Basi pepo mmoja alimwita mwenzake kwa sauti kubwa akasema: “Mwenzangu, twende kuoga maji!“ Pepo wa pili akamjibu, ikawa kama maiti yenyewe inajibu, akasema: “Sina nafasi kufuatana nawe, maana nimefikiwa na mgeni!“ Makari asiogope hata kidogo akatambua mchezo huu wa pepo. Akamgusa maiti ubavuni akasema: “Nenda tu ufuatane na mwenzako ukiweza kutoka hapa!“ Pepo waliposikia maneno haya walilia kwa ghadhabu wakasema:“Umetushinda! Umetushinda!“ Wakatoweka upesi.
Siku moja Makari alifikiwa na hawa vijana wawili. Mkubwa wao alianza kuota ndevu lakini wa pili alikuwa bado mvulana. Wakamwangukia Makari miguuni pake wakamwomba awarushusu kukaa kwake. Makari akawatazama akaona kuwa wote wawili wana miili laini sana. Akadhani kwamba hawataweza kustahimili taabu za jangwani, akawaambia akasema: “Hamwezi kukaa hapa kwangu, ndugu zangu!“ Wao wakamwuliza wakasema: “Tusipopata ruhusa kukaa kwako, basi, baba, tufanyeje?“ Makari akafikiri kwamba akiwafukuza watasikitika. Basi akawaambia akasema: “Basi, kaeni! Mjenge kijumba chenu mkiweza.“ Wakamwomba awaonyeshe mahali pa kujenga. Akawachukua akawaonyesha mwamba mkubwa akawapa vyombo na mashoka na kikapu cha mikate na chumvi akasema: “Kombeni mwamba huu. Baadaye mtengeneze paa. Miti iko huko kwenye mabwawa. Ikiwa nyumba ni tayari, basi mkae hapa!“ Makari alifikiri kwamba wataogopa kazi ngumu hii na watashindwa na watarudi nyumbani kwao. Vijana wakamwambia Makari wakasema: “Baba, utuonyeshe kazi tutakayofanya baadaye kama nyumba ni tayari!“ Basi Makari akachukua makuti akawaonyesha jinsi ya kusuka ukambaa na mikeka na vikapu. Halafu Makari akawaacha akarudi pangoni

kwake. Wanafunzi wale wakatimiza vizuri yote waliyoagizwa, lakini hawakumrudia Makari muda wa miaka mitatu.
Basi Makari akaanza kuhangaika akawaza moyoni mwake akasema: “Vijana wale wawili wanafanya nini? Mbona hawanifikii kuuliza neno. Wakaa pekee wengine wanaokaa mbali sana wanakuja kuuliza, lakini wawili hawa wanaokaa karibu hawafiki kwangu wala hawamendei mze mwingine. Ninawaona kanisani tu, wanapokea sakramenti takatifu na wanarudi kimya kijumbani kwao!“ Basi Makari akaanza kuwaombea, akafunga sana juma zima kwa ajili yao. Akamwomba Mungu amfumbulie hali zao. Juma lililopita akaondoka akawaendea wanafunzi wale ili awapeleleze. Akagonga mlango wao. Wakamfungulia mlango wakamwamkia kimya. Basi Makari akawabariki akaketi chini.
Kijana yule aliyekuwa mkubwa alimpungia mkono mdogo wake atoke nyumbani. Mkubwa akaketi chini akasuka kikapu kimya. Karibu ya saa tisa mkubwa yule akapiga ubao wa meza. Basi mdogo wake akaingia chumbani akaleta bakuli la uji. Mkubwa akaonyesha meza kwa mkono wake naye mdogo akaweka meza katikati ya chumba akaweka bakuli la uji pale pale na mikate mitatu, akaenda kusimama kidogo pembeni, asiseme neno. Basi Makari akamwambia mkubwa akasema: “Usimame, tule chakula chetu!“ Wakasimama wakala uji wakanywa maji.
Jioni vijana wote wawili walimwuliza Makari: “Baba, leo unarudi nyumbani kwako?“ Makari akawaambia akasema: “La, sikondoki leo, ila nitalala hapa kwenu!“ Wakamtandikia mkeka chumbani mle wakaweka mikeka yao pembeni kidogo. Saa ya kulala usingizi ilipokuwa tayari vijana walivua mishipi yao na ngozi zao walizovaa kwa ajili ya kazi wakalala chini. Pia Makari akajilaza penye mkeka wake, lakini hakulala usingizi, ila alisali akasema: “Ee Bwana, unifumbulie matendo yao.“
Pale pale ilikuwa kama paa la kijumba chao limefunguka na Makari aliona mwangaza mkubwa ulioangaza chumba chote. Lakini vijana hawakuona nuru hiyo. Wakajisingizia kulala usingizi lakini hawakulala. Baada ya muda mrefu kidogo walidhani kwamba Makari ameshikwa na usingizi, kumbe yeye aliwavizia. Basi mkubwa yule akamgusa mwenzake ubavuni. Wote wawili wakaamka kimya kabisa wakafunga mishipi yao. Baadaye walinyoosha mikono yao wakaiinua juu wakasimama hivi kiwimawima bila kutoa sauti. Makari akawaona kwa sababu ya mwangaza ule alioona peke yake, lakini vijana hawakuwona Makari kwa sababu ya giza la usiku. Basi Makari alipokuwa anawatazama walifika pepo wengi sana, kama kundi la mbu, wakamzunguka yule mdogo. Wengine walijaribu kuketi kwenye midomo yake na wengine walitaka kukaa katika macho yake. Basi akaja malaika mwenye

kushika upanga wa moto. Akawafukuza pepo akamkinga mdogo yule na masumbuo yao. Lakini pepo wote walishindwa kumkaribia kijana mwenzake aliyekuwa mkubwa. Karibu ya mapambazuko vijana hawa waajilaza tena chini juu ya mkeka wao. Baada ye Makari akajisingizia kwamba anaondokewa usingizi akaamka. Pia vijana wawili wakaamka. Basi mkubwa akamwambia Makari akasema: "Baba, ukipenda tunasali sasa zaburi kumi na mbili." Makari akaitikia, nao vijana wale wakapokezana kusali zaburi. Mzee Makari akastaajabu sana. Aliona kuwa mdogo akifumbua kinywa akisali ulimi wa moto ulitoka kinywani kwake na unapanda mbinguni. Kadhalika mkubwa akifumbua kinywa chake kwa kusali moshi wa manukato kama ubani na kama moto ulitoka kwake na kupanda mbinguni. Makari akawasaidia sala zao kwa moyo wake wote.

Asubuhi Makari akaaga kwao akawaomba wote wawili wamwombee kwa sala zao. Vijana wale wakaitikia kimya. Mzee Makari akarudi pangoni kwake. Alikuwa ametambua kwamba mkubwa wa vijana wale wawili ni mkamilifu na kwamba mdogo wake ni mkamilifu, lakini bado anashambuliwa na pepo. Zikapita siku chache tu mkubwa wa vijana wale akafa na baada ya siku tatu nyingine mdogo wake akamfuata. Tangu wakati ule Makari alipofikiwa na wakaa pweke kila mara amewachukua akaenda nao kwenye pango ya vijana wawili hawa akawaambia: "Tazameni, hapa walikaa vijana watakatifu!"

Siku moja Makari na wakaa pweke wa ujirani wake walisaidia kufyeka ngano katika shamba la mwenyeji na kufunga miganda. Nyuma yao alifuata mwanamke mjane naye aliokota masuke yaliyoanguka hali analia machozi. Basi Makari akamwuliza mwenye shamba akasema: "Kizee yule analia machozi kwa sababu gani?" Huyu akajibu akasema: "Bwana wake alikabidhiwa mali nyingi na mtu fulani ili aiweke vizuri. Basi bwana wake amekufa siku hizi hizi bila konyesha mahali alipoficha fedha ile. Mwenye mali anadai mali yake akatoa maneno ya ukali kwamba asipopata fedha yake atamwuza bibi yule pamoja na watoto wake kuwa watumwa. Amekwisha washika watoto wake." Makari akamwambia mwenye shamba akasema: "Umwambie mama yule kwamba anijie saa sita tunapopumzika kwa sababu ya joto la jua."

Basi Makari alipojiwa na mjane wakati wa kupumzika alimwuliza: "Kwa sababu gani unalia machozi kila wakati?" Mwanamke akamjibu akasema: "Bwana wangu kabla ya kufa kwake hakunionyesha mahali alipoficha mali aliyoaminishwa!" Makari akamwambia akasema: "Basi, unionyeshe kaburi la bwana wako!" Kizee yule akamtangulia Makari aliyefuatana na wakaa pweke wenzake saba akamwongoza kwenye kaburi. Pale Makari alimruhusu mwanamke kurudi nyumbani kwake. Wakaa pwekee wote wakapiga magoti

penye kaburi wakasali. Baadaye Makari alimwita marehemu kwa jina lake akamwuliza akasema: "Umeweka wapi mali ile uliyoaminishwa." Marehemu akajibu kutoka kaburini akasema: "Nimeiweka nyumbani kwangu chini ya kitanda upande wa miguuni!" Makari akamwambia marehemu akasema: "Basi, uendeleee sasa kulala kaburini hata siku watakapofufuka marehemu wote!"

Wakaa pweke wenzake walipoona jambo hili walimwangukia Makari miguuni pake wakashangaa sana. Makari akawaambia akasema: "Jambo hili halikutokea kwa ajili yangu nisiyefaa kitu, ila kwa ajili ya mama yule na watoto wake wakiwa. Bwana mwenyewe ameahidi kwamba tunapewa yo yote tunayoomba!" Basi wakaa pweke wote wakamwendea mjane nyumbani kwake naye Makari akamwambia mahali ilipowekwa mali ya mtu yule. Mwanamke akaichimbua akairudisha kwa mwenye mali akawakomboa watoto wake.

Siku moja Makari mdogo akavuka mto Nile pamoja na Makari mkubwa katika kivuko kimoja. Ikatokea kwamba akida wawili walikuwepo pia katika kivuko kile, pamoja na wale walioandamana nao. Akida hao walipowaona watakatifu wawili, waliovaa kimaskini, lakini waking'aa amani na utulivu usoni mwao, na dharau ya malimwengu, hawakuweza kutoambiana jinsi watumishi hawa wa Mungu walivyo heri kuishi maisha kama hayo. Na mmoja wao akawaambia: "Ninyi wawili ni wa heri, ninyi ambao ni juu ya ulimwengu na kuidharau miguuni mwenu." Makari mdogo akawajibu: "Kwa kutuita heri unazungumza kama unatoa unabii. Jina la kila mmoja wetu ndilo Makari, maana yake kwa lugha ya Kigiriki Heri. Lakini ikiwa unasema kweli kwamba wale walioacha vyote na kujiweka wakfu kwa ajili ya kumtumikia Mungu kwa kuyadharau malimwengu ni heri, tuna haki kuhurumia huzuni yenu ya kuwa watumwa wa ulimwengu huu na kutawaliwa nao." Maneno yake yaliingia moyoni mwa akida kwa nguvu, kiasi kwamba, aliporudi nyumbani, akaacha kazi yake, akagawa mali yake kwa maskini na kuanza maisha ya mkaa pweke.

Kwa kumaliza habari hizo nasimulia hadithi Mt. Hieronimo aliyoandika. Ikatokea kwamba mtawa mmoja wa Nitria aliyefanya kazi ya kutengeneza nguo aliweka akiba fedha nyingi. Alipofariki wakakuta kiasi cha solidii mia. Watawa wakakusanyika na kujadiliana namna gani fedha hiyo itumike. Wengine walisema, tuwaigawie maskini, wengine tujenge kanisa, wengine tuitumie kwa kuzika wafu. Lakini Makari, Pambo na Isidori, wakiangaziwa na Roho Mtakatifu, wakaamua kwamba fedha hizo zizike pamoja na maiti, wakirejea maneno ya Mt. Petro kwa Simoni mchawi: "*Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe*", Mdo 8:20. Na tukio hilo likasababisha hofu kubwa kati ya watawa wote katika nchi nzima ya Misri. Ilihesabiwa dhambi mtawa mmoja akiacha zaidi ya soldi moja wakati wa kifo chake.

Katika uzee wake siku moja Makari aliketi mlangoni pa kijumba chake. Alifikiri kwamba yeye alikuwa mtu mwenye uwezo kupita kiasi, akijiona shaibu, akijisikiliza anavyosema na kuyatenda. Alikuwa peke yake, mzee wa miaka mingi, kibogoyo. Alikuwa anashindana na nafsi yake. Alikuwa anasema: "Unataka nini wewe mzee mbaya? Tazama, unayo mafuta na umekunywa divai. Unataka nini, wewe mzee mlafi mwenye nywele nyeupe?" Na kwa Adui alisema: "Je, unanidai kitu gani? Hutapata kwangu kitu chochote ambacho ni mali yako, ondoka kwangu." Na kama alijinong'ona, akisema: "Tazama, wewe mzee mlafu mwenye nywele nyeupe, *nitakaa pamoja nawe hata lini?"* Mt 17:17.
Yasimuliwa kwamba tangu alipobatizwa, yaani kwa miaka sitini, hakutema tena mate chini. Alikuwa mfupi wa kimo na bila ndevu, wala nywele, isipokuwa midomoni mwake na katika ncha ya kidevu chake. Kwa sababu ya majikatalio yake makubwa nywele za ndevu yake hazikuanza kuota.
Makari alimtumikia Mungu upwekeni kwa uaminifu muda wa miaka hamsini. Alipotimia umri wa miaka mingi Bwana alimwita aende kupokea tuzo ya milele, mnamo mwaka 395. Makari anashiriki furaha za mbinguni na anamtukuza Mungu Baba na Mwana na Roho Mtakatifu hata milele. Amina.

*************